HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO

MUHTASARI WA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA MANISPAA TAREHE 30/04/2020

Wajumbe waliohudhuria

1.	Mhe. Pascal M. Kihanga	__	Mstahiki Meya -Mwenyekiti
2.	Ndg. Sheilla E. Lukuba	__	Mkurugenzi wa Manispaa -Katibu
3.	Mhe. Spear A. Komanya	__	Mjumbe
4.	Mhe. Zahara S. Kitima	__	Mjumbe
5.	Mhe. Ally R. Kalungwana	__	Mjumbe
6.	Mhe. Zamoyoni Juma Abdallah	__	Mjumbe
7.	Mhe. Hadija Kombo Kibati	__	Mjumbe
8.	Mhe. Wenceslaus Kalogeries	__	Mjumbe
9.	Mhe. Warda O.Bazia	__	Mjumbe
10.	Mhe. Amina H.Zihuye	__	Mjumbe
11.	Mhe. Suzana P.Mtikwa	__	Mjumbe
12.	Mhe. Mizambwa R.Lugonzo	__	Mjumbe
13.	Mhe. Daudi Salum Mnadi	__	Mjumbe
14.	Mhe. Msasa Hamisi Mohamedi	__	Mjumbe
15.	Mhe. Kuruthum Mwisongo	__	Mjumbe
16.	Mhe. Gilbert B.Mtafani	__	Mjumbe
17.	Mhe. Zinduna Kombo Selemani	__	Mjumbe
18.	Mhe. Gabriel M.Temba	__	Mjumbe
19.	Mhe. Kifimbo S. Jumanne	__	Mjumbe
20.	Mhe. Peter Joel Dhahabu	__	Mjumbe
21.	Mhe. Ndulu Castory	__	Mjumbe
22.	Mhe. Dismas W. Makanjira	__	Mjumbe
23.	Mhe. Amini Tunda Abdallah	__	Mjumbe
24.	Mhe. Mudhihiri S. Shoo	__	Mjumbe
25.	Mhe. Hassan Maringo	__	Mjumbe
26.	Mhe. Zawadi M.Kidando	__	Mjumbe
27.	Mhe. Juma A. Tembo	__	Mjumbe
28.	Mhe.Scolastica W. Mkude	__	Mjumbe
29.	Mhe. Hamisi A. Kilongo	__	Mjumbe
30.	Mhe. Rashid Matessa	__	Mjumbe
31.	Mhe. Hilda B.John	__	Mjumbe
32.	Mhe. Samuel Msuya	__	Mjumbe
33.	Mhe. Latifa Said Ganzel	__	Mjumbe
34.	Mhe. Mabula R. Lusewa	__	Mjumbe
35.	Mhe. Milikiel M.Mahiku	__	Mjumbe

36.	Mhe. Madaraka Bidyanguze	__	Mjumbe
37.	Mhe. Dorothy J.Mwamsiku	__	Mjumbe
38.	Mhe. Amiri Juma Nondo	__	Mjumbe

Wajumbe wasiohudhuria kwa taarifa.

1.	Mhe. Abdulazizi Mohamed (MB)	__	Mjumbe
2.	Mhe. Devotha Minja (MB)	__	Mjumbe
3.	Mhe. Dr. Christine Ishengoma (MB)	__	Mjumbe

Waalikwa waliohudhuria.

1.	Mhe. Regina R. Chonjo	__	Mkuu wa Wilaya ya Morogoro
2.	Ndg. Flora R. Yongoro	__	Kaimu Katibu Tawala Mkoa

Watendaji waliohudhuria

1.	Ndg. Enedy Mwanakatwe	__	Afisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa
2.	Ndg. Neema Michael	__	Mkaguzi wa Ndani wa Manispaa
3.	Ndg. Epiphania Matafu	__	Kaimu Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wa Manispaa
4.	Ndg. Chausiku Masegenya	__	Afisa Elimu Msingi wa Manispaa
5.	Ndg. Mbuke D. Dittu	__	Kaimu Mthibiti Mkuu wa Ubora wa Elimu wa Manispaa
6.	Ndg. Upendo Elias	__	Mratibu wa Kudhibiti UKIMWI wa Manispaa
7.	Ndg. Feliciana Katemana	__	Mratibu wa TASAF Manispaa
8.	Eng. Juma Gwisu	__	Mhandisi wa Ujenzi wa Manispaa
9.	Ndg. Samweli Subi	__	Kaimu Afisa Mazingira na Udhibiti wa Taka Ngumu wa Manispaa
10.	Ndg. Sadoth Kaijage	__	Mchumi wa Manispaa
11.	Ndg. Mohamed Chamzhim	__	Afisa Mifugo na Uvuvi wa Manispaa
12.	Dr. Ikaji Z. Rashidi	__	Mganga Mkuu wa Afya wa Manispaa
13.	Ndg. Kitutu Mshana	__	Afisa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano wa Manispaa
14.	Ndg. Winfred A. Kipako	__	AfisaTarafa wa Manispaa
15.	Ndg. Safia Kingwahi	__	Afisa Utamaduni wa Manispaa
16.	Ndg. Jafari A. Makupula	__	Afisa Ununuzi na Ugavi wa Manispaa
17.	Ndg.Dominica Ngaleka	__	Kny: Afisa Utumishi wa Manispaa
18.	Ndg. Gisbert Msemwa	__	Kaimu Afisa Mipangomiji na Maliasili wa Manispaa.
19.	Ndg. Elineema Mtaita	__	Katibu TSC wa Manispaa
20.	Ndg. Ponceano Kilumbi	__	Mweka Hazina wa Manispaa
21.	Ndg. Wilfred W.Mramba	__	Mwanasheria wa Manispaa
22.	Dk. Janeth Barongo	__	Afisa Elimu Sekondari wa Manispaa

23. Ndg. Festus Herman __ Afisa Biashara wa Manispaa
24. Ndg. Ana Kobero __ Afisa Utumishi

Sekretarieti

1. Ndg. Daudi A. Kibwana __ Katibu wa Mikutano
2. Ndg. Sylvia Kahitwa __ Katibu wa Mikutano
3. Ndg. Deogratias Butabile __ Katibu wa Mikutano
4. Ndg. Maria Leke __ Katibu wa Mikutano
5. Ndg. Theresia Mbena __ Katibu wa Mikutano
6. Ndg. Lilian Henerico __ Afisa Habari

HMM/BM/47/2019/2020 Kufungua Mkutano

Kabla ya kufungua Mkutano Mstahiki Meya aliomba Wajumbe wasimame kwa dakika 5 kumuombea dua marehemu Isiaka Sengo Mtandikile Naibu Meya wa Manispaa aliyefariki dunia tarehe 27/04/2020. Baadaye uliimbwa wimbo wa Taifa na Dua la kuiombea Halmashauri.

Mstahiki Meya aliwakaribisha Wajumbe na alifungua Mkutano saa 4:30 asubuhi. Baada ya Mkutano kufunguliwa Mstahiki Meya alimkaribisha Mkuu wa Wilaya ya Morogoro ili atoe salamu za Serikali.

Salamu za Mkuu wa Wilaya ya Morogoro

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro alitoa pole kwa msiba wa Marehemu Isiaka Sengo Mtandikile – Naibu Meya wa Halmashauri. Alimuombea Dua kwa Mwenyezi Mungu apumzike kwa Amani.

Kuhusu Stendi ya Kaloleni Kata ya Mji Mpya:-

Aliagiza kuwa mchakato wa kumpata Mkandarasi mwingine uharakishwe kwa kuwa Wananchi wanakosa huduma, aidha Mkandarasi wa awali Fast Construction Co. Ltd aliyelipwa fedha za awali **Tshs. 108,000,000.00** na kushindwa kazi achukuliwe hatua za kisheria.

Kuhusu Stendi ya Daladala Mafiga

Alishauri kuwa baadhi ya vitu visivyo vya lazima viondolewe ili kupeleka fedha kwenye huduma nyingine mfano vibanda vya mama na baba lishe.

Kuhusu kufungwa kwa Shule kipindi cha ugonjwa wa Corona

Alielekeza kuwa baada ya shule kufungwa kuanzia tarehe 16/03/2020 kwa sababu ya ugonjwa wa Corona Watoto/Wanafunzi wanarandaranda Mitaani hivyo kuwa na hatari ya kuambukizwa ugonjwa wa Corona, hivyo alieleza Waheshimiwa Madiwani wote wawaelimishe Wananchi wote kuwalinda Watoto wao watulie majumbani. Aidha, alisisitiza Wananchi kuendelea kuvaa barakoa na kutulia majumbani endapo hakuna sababu ya msingi ya kutembea.

Mkurugenzi wa Manispaa aliyachukua maelezo hayo na aliahidi kuyatekeleza.

HMM/BM/48/ 2019/2020 Kuridhia agenda za Mkutano.

Wajumbe waliridhia Agenda za Mkutano zifuatazo:-

1. Kufungua Mkutano.
2. Taarifa mbalimbali kutoka kwa Mkurugenzi wa Manispaa
3. Kusoma na kuthibitisha Mihtasari ya Mikutano ya Baraza la Madiwani ya tarehe 30/01/2020 (Mkutano wa kawaida), tarehe 17/02/2020 (Bajeti - Mapitio), tarehe 18/02/2020 (Bajeti 2020/2021).
4. Yatokanayo na Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani ya tarehe 30/01/2020 (Mkutano wa kawaida), tarehe 17/02/2020 (Bajeti - Mapitio), tarehe 18/02/2020 (Bajeti 2020/2021)
5. Taarifa za Kamati za kudumu na Kamati nyinginezo za Halmashauri.
    - 5.1 Kamati ya Fedha na Uongozi vikao vya tarehe 16/01/2020 (kawaida), tarehe 10/02/2020 (Bajeti), tarehe 17/02/2020 (kawaida), tarehe 29/02/2020 (Maalum), na tarehe 09/03/2020 (kawaida).
    - 5.2 Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya kikao cha kawaida cha tarehe 10/01/2020 na tarehe 20/01/2020 (Bajeti).
    - 5.3 Kamati ya Mipangomiji na Mazingira kikao cha kawaida cha tarehe 14/01/2020 na tarehe 28/01/2020 (Bajeti).
    - 5.4 Kamati ya Kudhibiti UKIMWI Kikao cha kawaida cha tarehe 13/01/2020 na tarehe 28/01/2020 (Bajeti).
    - 5.5 Kamati ya Maadili ya Madiwani.
6. Taarifa ya masuala ya Kiutumishi (agenda itawasilishwa kwenye kikao)
7. Kufunga Mkutano.

Aidha Wajumbe walikubaliana kuwa Agenda ya Maswali ya papo kwa papo kwa Mstahiki Meya na Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro isijadiliwe, Mjumbe mwenye maswali awasilishe kwa maandishi kwa Mkurugenzi wa Manispaa.

HMM/BM/49/ 2019/2020 Taarifa mbalimbali kutoka kwa Mkurugenzi wa Manispaa.

Mkurugenzi wa Manispaa alieleza kuwa hakuwa na taarifa yoyote ya kiserikali ambayo anapaswa kuiwasilisha Baraza la Madiwani

HMM/BM/50/ 2019/2020 Kusoma na kuthibitisha Mihtasari ya Mikutano ya Baraza la Madiwani ya tarehe 30/01/2020 (Mkutano wa kawaida), tarehe 17/02/2020 (Bajeti - Mapitio), tarehe 18/02/2020 (Bajeti 2020/2021)

Muhtasari wa Mkutano wa tarehe 30/01/2020

Masahihisho yalifanyika katika ukurasa wa 7 aya ya nne mstari wa nne baada ya neno nyingine iliongezwa sentensi "ikiwemo kujenga vibanda vya biashara. Aidha, Mradi utaisha tarehe 30/06/2020 kazi ipimwe na taarifa itolewe Kamati ya Fedha na Uongozi.

Baada ya masahihisho hayo mihtasari ilithibitishwa kwa kusainiwa na Mwenyekiti na Katibu kuwa kumbukumbu sahihi za Mikutano

HMM/BM/51/ 2019/2020 Yatokanayo na Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani ya tarehe 30/01/2020 (Mkutano wa kawaida), tarehe 17/02/2020 (Bajeti - Mapitio),

a) Yatokanayo ya tarehe 31/01/2020

1.0 Kuhusu Gharama za mradi kuwa kubwa kwenye baadhi ya maeneo katika stendi ya daladala Mafiga.

Azimio

Baraza liliamua kuwa vifaa/kazi zilizopangwa kwenye mkataba zisipunguzwe ila ziendelee kutekelezwa na Menejimenti iendelee kupunguza gharama ili kupata fedha ambazo zitatumika kufanya kazi nyingine ikiwemo ujenzi wa Vibanda vya biashara.

Aidha, Mradi utaisha tarehe 30/06/2020 hivyo kazi ipimwe na taarifa itolewe Kamati ya Fedha na Uongozi. Kamati ya Fedha na Uongozi iliagizwa ifanyie kazi maelekezo hayo.

Utekelezaji

tarehe 18/02/2020 (Bajeti 2020/2021)	Azimio litazingatiwa kama ilivyoelekezwa na Baraza.	
	Mjadala Ilielezwa kuwa kazi hiyo iendelee kufanyika na kuzingatia ukomo wa muda wa matumizi wa fedha za Miradi ya ULGSP unaoisha tarehe 30/06/2020.	
	Kuhusu kiasi cha fedha kitakachookolewa katika Mradi wa Stendi ya Daladala Mafiga. **Agizo** Baraza liliagiza taarifa iwasilishwe katika kikao cha Kamati ya Fedha na Uongozi ili kujua ni kiasi gani kimeokolewa na kazi zitakazofanyika ikiwa ni pamoja na idadi ya Vibanda vya Biashara vitakavyojengwa.	
2.0	**Kuhusu vikundi kazi vya Usafi wa Mazingira vinavyodaiwa tripu za kuzoa taka ngumu** Baraza liliagiza kuwa vikundi sita vya usafi wa mazingira vilivyokopeshwa tripu za kubeba taka ngumu Menejimenti iendelee kuvifuatilia ili vilipe.	
	Utekelezaji Hadi tarehe 20/03/2020 vikundi 3 vilikuwa bado vinadaiwa **Tsh. 1,260,000.00**. Kiumu Cleaners **Tsh. 450,000.00**, Msimamo **Tshs. 750,000.00** na Mwale Cleaners **Tshs. 60,000.00**.	
	Agizo Menejimenti iliagizwa kuendelea kufuatilia vikundi vinavyodaiwa tripu za kuzoa Taka na kuweka ukomo wa muda wa malipo hayo, kikundi kitakachokaidi kichukuliwe hatua za kisheria.	
3.0	**Kuhusu vibali vya ujenzi na uvamizi wa maeneo ya wazi** **Azimio** Kamati ya Mipangomiji na Mazingira ishughulikie changamoto ya ujenzi holela mjini, watu waliojenga bila kuwa na vibali vya ujenzi na waliovamia na kujenga kwenye viwanja vya matumizi ya wazi na kuwasilisha taarifa kwenye mkutano ujao.	
	Utekelezaji Agizo limezingatiwa. Kamati ya Mipangomiji na Mazingira katika kikao chake cha tarehe 14/01/2020 iliunda Kamati Ndogo ya kushughulikia suala hilo na taarifa itawasilishwa katika Kamati hiyo kisha Baraza la Madiwani	
	Mjadala Baraza lilipokea na kuridhia majibu kwa ajili ya utekelezaji.	

4.0 Kuhusu kutoza kodi kwenye kumbi za mikutano na sherehe

Azimio

Baraza iliiliagiza kuwa tozo za sherehe za ukumbini zitozwe kwa asilimia ya kiasi anacholipa anayekodishiwa badala ya shilingi 20,000.00. Menejimenti ifanyie kazi asilimia itakayotozwa na kuwasilisha taarifa mkutano ujao

Utekelezaji

Tozo kwa kuzingatia asilimia 10 kwa anayekodisha limeanza kutekelezwa.

Wahusika wanaelimishwa na wanalipa kwa kuzingatia agizo hilo.

5.0 Kuhusu Mapato ya Maegesho

Azimio

Menejimenti iharakishe kufanya kikao na TARURA ili kubainisha maeneo ambayo Halmashauri na TARURA wanapaswa kukusanya.

Utekelezaji

Timu ya Wataalam kati ya Manispaa ya Morogoro na TARURA ilikaa tarehe 24/04/2020 ili kujadiliana vituo vitano (5) vinavyopaswa kukusanywa na Manispaa. Vituo hivyo ni eneo la wazi Mawenzi (kituo cha Bio gas), Manzese eneo la wazi, SIDO, Lupila, na Goldland/Step 1.

Baada ya maeneo hayo kuainishwa na majadiliano kufanyika TARURA ilikataa mapendekezo ya maeneo hayo kukusanywa na Manispaa, aidha Menejimenti imeitaka TARURA itoe majibu hayo kwa barua.

Mjadala na Maamuzi

Agizo

Baraza liliagiza Menejimenti iendelee kushauriana na TARURA ili kuacha maeneo hayo yakusanywe na Halmashauri ya Manispaa.

b) Yatokanayo ya tarehe 17/02/2020

1.0 Kuhusu umaliziaji wa Zahanati na vituo vya Afya vya Halmashauri

Azimio

Baraza lilimuagiza Mkurugenzi wa Manispaa atafute fedha za kumalizia ujenzi wa vituo vya Afya na Zahanati zilizoanza kujengwa. Aidha Menejimenti iendelee kufuatilia fedha za maendeleo Serikali Kuu ili ziletwe na kukamilisha miradi ya maendeleo.

Utekelezaji

Zahanati na Vituo vya Afya vilivyotengewa fedha katika bajeti ya 2019/2020 vinaendelea kupelekewa fedha kadri zinavyopatikana, aidha, katika bajeti ya mwaka 2020/2021 suala hili limezingatiwa.
Vilevile Halmashauri imeomba maombi maalum kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya **Tshs. 1,500,000,000.00** na vituo vya Afya (Mafisa, Sabasaba na Lukobe – Kituo Kipya) **Tshs. 1,500,000,000.00** Jumla Kuu **Tshs. 3,000,000,000.00**

Mjadala
Wajumbe walimpongeza Mstahiki Meya na Mkurugenzi wa Manispaa kwa kusimamia Mapato vizuri.

Kuhusu Wodi ya Wazazi ya Regina Chonjo katika Kituo cha Afya Sabasaba.
Baraza la Madiwani lilielekeza kijengwe chumba cha upasuaji (Theatre) katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021.

Ufafanuzi
Menejimenti ilieleza kuwa suala la ujenzi wa chumba cha upasuaji limewekwa kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo litapewa kipaumbele wakati wa utekelezaji wa bajeti hiyo.

Sanjari na hayo Baraza la Madiwani liliazimia kuwa wakati wa utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Vituo vya Afya vyenye Wodi ya Wazazi viwekewe mitungi ya gesi.

Ufafanuzi
Ilifafanuliwa kuwa Menejimenti imelipokea suala hilo kwa ajili ya utekelezaji.

HMM/BM/52/ 2019/2020 Taarifa za Kamati za kudumu na Kamati nyinginezo za Halmashauri.	**1.0**	**Kamati ya Fedha na Uongozi vikao vya tarehe 16/01/2020 (kawaida), tarehe 10/02/2020 (Bajeti), tarehe 17/02/2020 (kawaida), tarehe 29/02/2020 (Maalum), na tarehe 09/03/2020 (kawaida).** Taarifa iliwasilishwa, ilipokelewa na kuridhiwa na Baraza la Madiwani.
	2.0	**Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya kikao cha**

kawaida cha tarehe 10/01/2020 na tarehe 20/01/2020 (Bajeti).
Taarifa iliwasilishwa, ilipokelewa na kuridhiwa na Baraza la Madiwani.

3.0 Kamati ya Mipangomiji na Mazingira kikao cha kawaida cha tarehe 14/01/2020 na tarehe 28/01/2020 (Bajeti)
Taarifa iliwasilishwa, ilipokelewa na kuridhiwa na Baraza la Madiwani.

4.0 Taarifa ya Kamati ya Kudhibiti UKIMWI Kikao cha kawaida cha tarehe 13/01/2020 na tarehe 28/01/2020 (Bajeti).
Taarifa iliwasilishwa, ilipokelewa na kuridhiwa na Baraza la Madiwani.

5.0 Taarifa ya Kamati ya Maadili ya Madiwani
Taarifa iliwasilishwa, ilipokelewa na kuridhiwa na Baraza la Madiwani.

HMM/BM/53/2019/2020 Taarifa ya Masuala ya Kiutumishi

Baraza lilijigeuza kuwa Kamati na kujadili masuala ya kiutumishi.
Ilielezwa kuwa Ofisi imepokea barua yenye Kumb. Na. CCD.273/361/01/C/61 kutoka kwa Katibu Mkuu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ya tarehe 17/12/2019 iliyojibu barua yenye Kumb. Na. MMC/CM.10/17//VOL.II/148 ya tarehe 16 Julai, 2019.

Barua hiyo iliitaka Manispaa kuendelea na zoezi la Uteuzi wa **Bw. Samweli Maduhu Subi** kuwa Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira baada ya zoezi la upekuzi uliofanywa na Ofisi ya Katibu Mkuu kukamilika. Aidha katika upekuzi huo ilibainika kuwa hana dosari zozote za kiusalama, kiutendaji wala kitabia.

Kwa Mamlaka ya Halmashauri iliyonayo chini ya kifungu cha 6(1)(b) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma imeitaka Halmashauri kuendelea na mchakato wa Uteuzi na kutoa taarifa kwake.

Maoni ya Kamati ya Fedha na Uongozi
Kamati ya Fedha na Uongozi katika kikao chake cha kawaida cha tarehe 17/02/2020 ilipitia mapendekezo hayo na iliridhia kwa hatua zaidi.
Hivyo, Menejimenti iliwasilisha jina la **Bw. Samweli Maduhu Subi** ili Baraza la Madiwani liweze kutoa Mapendekezo ya kuridhia Mtumishi huyo kuwa Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira ili jina lake liwasilishwe tena kwa Katibu Mkuu (Utumishi) na hatimaye kwa Katibu Mkuu Kiongozi kwa hatua zaidi.

Taarifa binafsi za Bw. Samweli Maduhu Subi ziliwasilishwa.

Maamuzi ya Baraza la Madiwani

Baraza la Madiwani lilipokea na kuridhia Mapendekezo na kumuidhinisha **Bw. Samweli Maduhu Subi** kuwa Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira, ili jina lake liwasilishwe kwa Katibu Mkuu (Utumishi) na hatimaye kwa Katibu Mkuu Kiongozi kwa hatua zaidi.

HMM/BM/54/ 2019/2020 Kufunga Mkutano

Mstahiki Meya aliwashukuru Wajumbe kwa kuchangia hoja mbalimbali na kusisitiza ushirikiano kwa maendeleo ya Halmashauri. Alifunga Mkutano saa 5: 16 Asubuhi.

Muhtasari umethibitishwa tarehe ……

……..	…….
Mhe. Pascal M. Kihanga	Ndg. Sheilla E. Lukuba
MSTAHIKI MEYA	**MKURUGENZI WA MANISPAA**
MWENYEKITI	**KATIBU**

YATOKANAYO NA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 30/04/2020

MUHT. NA.	AZIMIO	MTEKELEZAJI	UTEKELEZAJI
HMM/BM/51/ 2019/2020 Yatokanayo na Mikutano ya Baraza la Madiwani ya tarehe 31/10/2019 (kawaida) na tarehe 27/12/2019 (maalum).	**1.1 Kuhusu kiasi cha fedha kitakachookolewa katika Mradi wa Stendi ya Daladala Mafiga.** Baraza liliagiza taarifa iwasilishwe katika kikao cha Kamati ya Fedha na Uongozi ili kujua ni kiasi gani kimeokolewa na kazi zitakazofanyika ikiwa ni pamoja na idadi ya Vibanda vya Biashara vitakavyojengwa.	Meneja TARURA Manispaa	Agizo limezingatiwa kiasi cha fedha **Tshs. 132,258,526.00** kimeokolewa. Aidha, kazi ya ujenzi wa vibanda **30** umeanza kutekelezwa kwa njia ya force akaunti.
	2.0 Kuhusu vikundi kazi vya Usafi wa Mazingira vinavyodaiwa tripu za kuzoa Taka Ngumu. Menejimenti iliagizwa kuendelea kufuatilia vikundi vinavyodaiwa tripu za kuzoa Taka na kuweka ukomo wa muda wa malipo hayo, kikundi kitakachokaidi kichukuliwe hatua za kisheria.	Afisa Mazingira na Udhibiti wa Taka Ngumu wa Manispaa.	Ukomo wa kulipa madeni ya kubebewa taka n magari ya Manispaa ni tarehe 10/06/2020, baada ya hapo hatua z kisheria zitachukuliwa hadi tarehe 29/05/2020 vikundi 6 vilikuwa vinadaiwa Tshs. 1,460,000.00. Uwamamo 200,000.00, Assembly 400,000.00, Watama 200,000.00, Msimamo 750,000.00, Uvume 230,000.00, na Juhudi 40,000.00

	3.0 Kuhusu maeneo ambayo yanamilikiwa na Manispaa (eneo la wazi Soko l Mawenzi kituo cha Biogasi, eneo la wazi Manzese, SIDO, Lupila na Goldland/step 1) ambayo TARURA inakusanya ushuru wa maegesho. Baraza liliagiza Menejimenti iendelee kushauriana na TARURA ili kuacha maeneo hayo yakusanywe na Halmashauri ya Manispaa.	Mweka Hazina wa Manispaa	Maeneo hayo TARURA wamekataa kuyaacha kwa Manispaa, tayari wamemuweka Mzabuni wa kukusanya maeneo hayo.